

NJIA ILIYOWEKWA NA MUNGU KWA AJILI YA SIKU HII

 ...Maandiko. Hakika ninafuraha kuwa na ninii, nyuma yangu usiku huu...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Fungueni Maandiko, kwa ajili ya fungu dogo tu la maneno, Bwana akipenda.

² Pia kumbukeni, kesho usiku, tunawaombea wagonjwa tena. Na sasa wakati nikizungumza...Sikilizeni, kila mtu ajaribu kufanya jambo hili, msingojee jambo fulani lolote kutukia. Jambo mnalopaswa kufanya, ni kumwamini Mungu sasa hivi. Mwaminini sasa hivi! Unaona?

³ Sasa kumekuwako na huduma nyingi za kila namna. Mungu, katika siku hizi za mwisho, ninaamini, ametupa kila kitu alichonacho kwenye Kitabu Chake. Kila kitu alichohaidi, tumekiona, na ingali inaonekana kana kwamba watu hawawezi kushika jambo hilo. Wale walioachaguliwa kulishika, watalishika; ni hao tu. Linampofusha mtu mmoja; linayafungua macho ya mwingine.

⁴ Kumbuka, tunaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Si kwamba amekufa, bali yu hai milele. Naye yupo hapa usiku wa leo. Tupo katika Uwepo Wake, usiku huu, Naye yupo hapa kuthibitisha na kutimiza ahadi yoyote ambayo alitoa kwa ajili ya siku hii. Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa hiyo, chochote yeye alichokuwa, ndicho alichokuwa usiku huu. Kwa hiyo hebu na tumwamini sasa, tunaposoma Neno Lake na kuzungumza habari Zake, kwa dakika kumi na tano, ishirini zifuatazo.

⁵ Mwanzo, mlango wa 22, na kifungu cha 7 na cha 8, kwa njia ya kupata somo.

Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babaangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa?

Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.

⁶ Bwana Yesu, libariki Neno Lako, jalia lisirudi bure, bali jalia hizo mbegu zianguke kwenye udongo ambapo itawaletewa wokovu hao walio na haja, kimwili na kiroho pia. Tunajikabidhi Kwako; kusanyiko, wasikilizaji, Neno, somo, yaliyomo. Jalia

Roho Mtakatifu na atwae utu wa kila mmoja wetu, kusudi tupate kumwona Yesu Kristo. Amina.

⁷ Ninataka kuzungumza kwa dakika chache tu zifuatazo sasa juu ya: *Njia Iliyowekwa na Mungu Kwa Ajili ya Siku Hii*.

⁸ Mungu daima amekuwa na njia. Zipo njia mbili, hizo ni, njia zetu au njia Zake. Mungu ana njia kwa ajili ya siku hii, kwa kuwa Yeye daima amefanya njia kwa ajili ya kila kitu. Mungu, hapo mwanzo, alijua mwisho, kwa hiyo ameweka Maandiko Yake kwa ajili ya kila kipindi cha wakati. Na wakati huo, unapofika... Sasa usikose kuona jambo hili. Wakati huo, unapofika, kwa kawaida huduma imechanganyikiwa sana katika itikadi, na kadhalika, na desturi, mpaka inakuwa mamilioni ya maili mbali na Neno.

⁹ Na ndipo Mungu sikuzote humtuma mtu fulani jukwaani, nabii. Na nabii huyu... Mungu kamwe habadilishi mfumo Wake. Habadilishi njia Zake kamwe. Yeye daima hufanya jambo hilo kwa namna ile ile. Daima amefanya hivyo; Hana budi kufanya jambo hilo wakati huu. Na, kwa kupitia jambo hili, Mungu hutenda kazi na kuthibitisha Neno hilo. Kama nilivyoongea nanyi jana usiku, Mungu akijifasiria Mwenyewe. Mungu hahitaji mtu yeyote kumfasiria Neno. Yeye hulifasiria Mwenyewe, kwa kulithibitisha, kulifanya halisi. Na Mungu anaposema atafanya jambo fulani, basi Yeye hulifanya, hakuna tena swali kwa hilo. Hivyo ndivyo anavyofanya mambo.

¹⁰ Kwa hiyo Mungu ametutengenezea njia. Mungu anawapenda watoto Wake. Anawapenda watu Wake. Anataka kuwasaidia. Yeye anataka kukusaidia wewe zaidi ya vile unavyotaka usaidizi. Laiti ungeweza kupata hilo moyoni mwako, ya kwamba Mungu yuko tayari kukusaidia zaidi ya vile unavyotaka kujisaidia mwenyewe. Lakini ana njia, na hiyo ndiyo njia pekee ambayo Yeye atatumia ni kwa kupitia kwa njia Yake. Huna budi kutimiza masharti Yake, si masharti yako. Masharti Yake! Wewe unalitaka kwa njia fulani, bali Yeye—Yeye anakupa hilo kwa njia Yake.

¹¹ Kama vile Naamani kujitumbukiza kwenye—kwenye—kwenye maji ya Yordani. Mbona, yeye alisema maji ya huko nchini kwake ni masafi sana na ni mazuri zaidi, lakini hivyo sivyo nabii alivyosema. “Jitumbukize hapa.” Akajitumbukiza mara moja, ukoma ungali upo; mara sita, ukali ulikuwa pale. Ilimbidi atii na alijie kwa njia ya Mungu. Ndipo wakati alipoitii njia ya Mungu kikamilifu, ukoma uliondoka.

¹² Nami ninasema, usiku wa leo, ya kwamba kama tukitii njia iliyowekwa na Mungu, ukoma utaondoka, magonjwa yataondoka, kila kitu kitaondoka, bali hatuna budi kupitia kwenye njia Yake kwa siku hii. Sasa, kujitumbukiza katika Yordani hakungesaidia kitu sasa; huko kulikuwa ni kwa ajili ya

Naamani. Torati ilikuwa ni kwa ninii—kwa ajili ya Wayahudi. Neema ni kwa njia ya Kristo.

¹³ Lakini kila wakati una sehemu yake ya Injili iliyotabiriwa tayari. Biblia hii ni ufunuo mzima wa Yesu Kristo. Hakuwezi kuwepo tena na mengine ya kuongezewa Kwake, wala chochote cha kuondolewa Kwalo; mtu anayefanya jambo hilo amelaaniwa. Hatuwezi kuongeza neno Kwalo, wala kutoa neno Kwalo. Hatuna budi kuangalia ndani hapa na kuona kilichoahidiwa kwa ajili ya wakati huu, na kisha tukione kikitukia. Huyu ni Mungu akifasiri Neno Lake Mwenyewe. Liliposema, “Bikira atachukua mimba,” alichukua mimba. Hiyo ni tafsiri ya Mungu ya jambo Hilo. Anachoahidi, Yeye hukitimiza.

¹⁴ Sasa tunaona ya kwamba Mungu habadilishi taratibu Zake za kufanya mambo. Yeye sikuzote hufanya jambo hilo jinsi hiyo hiyo. Sisi tunabadilika daima kwa kuwa sisi tuna mipaka. Tunafanya makosa ya kila namna, na tunaweza kufanya vizuri zaidi na kuwa bora zaidi. Lakini Mungu hana mpaka. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu wakati wote. Hawezi kupata ujuzi zaidi. Alikuwa ninii... Yeye ni chimbuko la ujuzi wote. Yeye ni hekima yote. Yeye ni mwenye nguvu zote, mweza yote, yuko kila mahali, anajua yote, na hana kikomo. Kwa hiyo basi, anaposema jambo lolote, shikilia nafsi yako kwa jambo Hilo, kwa maana ni kweli.

¹⁵ Sasa baadhi ya makanisa husema, “Nasi hatuamini jambo *Hili*, na tunaamini jambo *lile*.” Mungu kamwe hatauhukumu u—ulimwengu kwa kanisa fulani. Yeye huuhukumu kwa Yesu Kristo, na Yesu ni Neno. Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Neno.

¹⁶ Na iwapo *Huu ni* ufunuo wa Yesu Kristo kwa nyakati zote, na kwa wakati huu, Yeye amefunua katika Biblia hii yale ambayo angefanya katika wakati huu; na tunapooni Hilo likifanyika, tunapomwona Yeye akifanya yale aliyoahidi kufanya. Si kuzaliwa na bikira; huko kulikuwa ni miaka elfu mbili iliyopita. Bali ni yale aliyoahidi kufanya leo, yale aliyosema angefanya leo, hivyo ndivyo Yeye alivyo leo.

¹⁷ Mara nyingi, watu husema, “Vema, siamini jambo Hilo.” Vema, wewe una mfasiri wa Hawa tena; anachukua tu sehemu yake, bali si lote.

¹⁸ Kwa hiyo tunataka kukumbuka ya kwamba Mungu daima hudumu vile vile. Neno Lake, na yale anayosema, Yeye atayatimiza.

¹⁹ Kuonyesha ya kwamba Yeye habadiliki. Katika Mwanzo 1, Yeye alisema, “Na kila mbegu na izee kwa jinsi yake. Na kila mbegu na izee kwa jinsi yake.” Na papo hapo, tunafikia kwenye kitu fulani papo hapo kinachowabwaga chini wanadharia wa wanamageuzi ya polepole. Huwezi kuzalisha vitu tena. Hebu chukua kwa mfano farasi na—na ninii...na

pu—punda, wazalishe pamoja, unampata nyumbu, bali nyumbu hawezi kuzaa tena na azae nyumbu mwingine. Anakoma papo hapo. “Kila mbegu kwa jinsi yake.” Wanaweza kuzalisha, bali inajibadilisha na kurudia tena hali ya kwanza, inaonyesha ya kwamba haigeuki namna hiyo. La, bwana. Inakoma papo hapo. Unaweza kuzalisha mchicha na kitu kingine, pamoja, na kupata sukumawiki, bali huwezi kuzalisha hizo tena. La, bwana. Unaweza kuzalisha mahindi ya haibridi; bali ukipanda mahindi hayo ya haibridi tena, hutapata kitu. Inakubidi kurudia kuyazalisha kila wakati. Kwa sababu, Mungu alisema, “Na kila mbegu ize kwa aina yake.”

²⁰ Na sasa, kwa kuhaibridi vitu, angalia ulimwengu umetumbukia wapi leo. Nilikuwa nikisoma makala fulani hapa, kutoka kwenye *Reader's Digest*, ambapo, “Miaka ishiri tangu sasa, wanawake hawatazaa watoto, kama ikiendelea. Wanakula chakula cha haibridi.” Jambo lenyewe ni kwamba, wamechanganya mbegu, wala hivyo sivyo mwanadamu alivyoubwa, kula chakula cha aina hiyo. Alifanywa kukikuta kwenye... ama kukila jinsi kilivyoubwa. Hiyo ndiyo sababu, leo, kwamba hawawezi kuweka nyama na kila kitu jinsi ilivyo, ni kwa sababu ni ya haibridi, imepandwa kwenye mazingira yasiyo ya asili, na, loo, njia ya kila namna. Kila kitu kimechanganywa tu. Imefikia mahali ambapo jamii nzima ya binadamu inaangamizwa na mafanikio yao wenyewe, kwa kujaribu kuchukua kitu ambacho Mungu alikifanya vizuri, na kukigeuza na kukifanya kiwe cha namna nyingine, katika njia yao wenyewe. Kiache jinsi Mungu alivyokiumba!

²¹ Hata imefikia mahali ambapo wao wanajaribu kuhaibridi makanisa, leo; kutoka kwenye ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu, ukawa ni kupeana mikono; namna fulani ya kunyunyizia maji, kuwa ubatizo wa maji. Loo, jamani! kitu hicho chote ni haibridi. Tunataka kurudi.

²² Mmea wa haibridi, inakubidi kuubembebeza na kuupiga dawa, na kuwafukuza wadudu na mende watoke kwake. Bali huo si mmea halisi wenye afya; wenyewe ni imara, una nguvu, wala hakuna wadudu wowote wanaouvamia. Una ya kutosha ndani yake kumfukuza mdudu toka kwake.

²³ Na ndivyo ilivyo na Mkristo halisi! Haikubidi kumbembebeza na kumdekeza, na kumwambia *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Ana kitu ndani yake, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao hutupilia mbali mengine yote. Haikulazimu kumsihisihi, kwa kuwa yeye ni mmea halisi wa Mungu. Ana kitu ndani yake kinachopigana vita. Mkristo hupigania sehemu yote ya nchi anayosimama. Inampasa kufanya hivyo, kama anatarajia kuishi. Na, kwa kufanya jambo hilo, kuna kitu Fulani ndani yake kinachomlinda.

24 Hawa alijaribu kuhaibridi Neno, hapo mwanzo. Mungu alimwambia, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Alijaribu kulizalisha na maarifa aliyopewa na Shetani. Na alipofanya hivyo, akapoteza jamii nzima ya binadamu, pale pale, kwa ibilisi, alipojaribu kuchanganya Neno la Mungu lisiloghoshiwa na maarifa. Halitolewi na maarifa ya ulimwengu.

25 Linatolewa na nguvu za Roho Mtakatifu! “Si kwa nguvu, kwa uweza, bali kwa Roho Yangu,” asema Bwana. Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya jambo hilo. Neno la Mungu ni mbegu ya Uzima wa Milele.

26 Ukijaribu kulihaibridi, utafanya nini? Utajiua nalo. Halitafanya kazi. Halitachanganyikana tena zaidi ya vile mafuta ama maji yalivyowahi kuchanganyikana. Halitafanya hivyo.

27 Hawajaweza kamwe, wakati wowote, kufanya jaribio lolote lililofanikiwa ambalo ni bora kuliko njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Mwajua, hawajawahi kupata njia, bora, kwa kuku kuzaliwa uliwenguni humu, kuliko kudonoa mwenyewe ajitoe katika ganda lake. Je! uliwahi kujua jambo hilo? Kamwe hawajapata njia bora zaidi. Maskini jamaa huyo anazaliwa na pua ndogo kama ya nguruwe mwishoni mwa ninii yake—mwishoni mwa mdomo wake. Na kijidomo hicho alichu nacho, kuingia nacho kazini na kuanza kuchakura, kuchakura-chakura, mpaka anaanza kutokeza kichwa chake, anatokeza kichwa chake nje, anajitokeza na kuwa huru. Ndiyo njia iliyotolewa na Mungu. Ukimvuta kutoka kwenye hilo ganda, itamwua. Hataishi kama ukimvuta kumtoa kwenye hilo ganda. Inabidi aje kwa njia ya Mungu.

28 Hiyo ndiyo shida ya Wakristo siku hizi. Tumewabembeleza sana, tuliwapa mikono na kuwaingiza kisiri, na kuwaunganisha na kanisa. Wanachohitaji ni madhabahu ya mtindo wa kale ya maombi ambapo wataomba wapate ushindi, mpaka wakijitegemea wenyewe, waingie katika njia iliyowekwa na Mungu, mpaka watakapojiweka huru na ulimwengu. Shida yake, siku hizi, wanaandika jina lao katika kitabu na kujiunga na kanisa, na ni hayo tu. Bali njia ya Mungu, aliyoandaa, ni kukaa hapo na kujitahidi ufaulu, mpaka Mungu akupe Kuzaliwa upya. Hiyo ni kweli kabisa. Ukimshika umtoe nje, jambo hilo litamwua.

29 Hiyo ndiyo shida, leo hii, na watu. Kuzaliwa upya, wote wanakukwepa. Hawakutaki. Loo, wameweka kitu fulani badala ya Kuzaliwa upya, “njoo na uamini, na hivyo ndivyo tu inavyokubidi kufanya.” Ibilisi anaamini, yeye mwenyewe, nanyi mnajua yeye hajazaliwa mara ya pili. Kuna Kuzaliwa upya. Kuna kitu fulani kinachoambatana nako, kwa namna fulani hakifai, hakina ladha nzuri kwa ulimwengu.

³⁰ Uzazi wowote ni machafuko. Sijali unafanyika wapi. Kama uko katika kizizi cha nguruwe, ama—ama hospitalini. Uzazi ni machafuko.

³¹ Ndivyo kulivyo kuzaliwa upya! Kutafanya ufanye mambo hukufikiria ungefanya. Kutakufanya ushuke madhabahuni na ulie, upige kiyowe, uoshe rangi kutoka usoni mwako, uinue mikono yako, umisifu Mungu, unene kwa lugha, na mambo yote ya kila namna. Kuzaliwa upya kutafanya hivyo kwa sababu ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu ya kuzaliwa mara ya pili.

³² Huna budi kufa. Inakulazimu kufa kabla ya kuzaliwa tena. Mbegu yoyote inapaswa kufa kabla ya kuzaliwa mara ya pili. Isipokufa, itakaa peke yake. Mtu anapaswa kufia mawazo yake mwenyewe. Anapaswa kufia mawazo ya jambo lolote lile kuacha Neno la Mungu, na mtu huyo aje kwa njia Yake. Hayo ndiyo masharti ya Mungu. Hatukutani Naye kwenye mawazo yetu; tunakutana Naye kwa yale aliyosema ufanye. Hiyo ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Watu huipea; hawaitaki. Lakini ni ya kweli, hata hivyo. Itaninii, inasababisha mauti, nawe huna budi kufa, kufia mawazo yako.

³³ “Vema, ninajua Biblia inasema jambo hilo, bali siwezi kulifahamu.” Basi kaa pale mpaka Mungu atakapofunua jambo hilo. Hiyo ni kweli. Halina budi. . . Huko ndiko Kuzaliwa upya.

³⁴ Mabata na mabata bukini, kamwe hawajapata njia yao iliyo bora zaidi kwenda Kusini, kuliko kwanza kukusanyika. Na hiyo ni kweli. Utawaona wote wakikusanyika, nao watakusanyika wenyewe, namna fulani ya silka inawavuta pamoja, nao wanakusanyika na kusongamana kabla ya kuruka, kabla ya kwenda Kusini. Ni kitu gani? Ni wakati wa ufufuo, wakati hao wote watakapokusanyika. Je! ulipata kusikia makelele ya ndege kama hayo maishani mwako, kama kuwasikia hao mabata bukini wakikusanyika pamoja, ama hao mabata? Sijapata kusikia kitu kama hicho! Nao wananinii. . . Hakuna nyingine, njia nyingine ya wao kufanya jambo hilo.

³⁵ Mara nyingi, huko kwenye misitu ya kaskazini, ninachunguza mwanzo wa msimu wa baridi, huko Canada. Kundi la mabata waliozaliwa kule kule kwenye ziwa lile, hawajapata kutoka humo ziwani, jamaa huyu mdogo hajapata kutoka. Na muda si muda wajua, upepo wa baridi unashuka kutoka Kaskazini. Maskini huyu bata mdogo dume, yeye amezaliwa tu akiwa ni kiongozi, anatoka anaenda moja kwa moja huko nje katikati ya kidimbwi hicho, anatupa mdomo wake hewani, analia mara nne ama tano, na kila bata hapo majini anakuja kwake moja kwa moja. Naye anainuka kutoka pale, na anaenda moja kwa moja mpaka Louisiana awezavyo kwenda, kwenye mashamba ya mpunga.

³⁶ Kwa nini? Hawajawahi kamwe kupata njia bora zaidi kwa yeye kufika kule. Huwezi kuwakusanya pamoja. Ukiwaweka

kwenye nundu na...kwenye tundu, na kuwabeba kwenye lori kule. Bata huyo anajua vema zaidi jambo hilo. Na ukimweka kwenye tundu hilo, upate kumpeleka kule chini, yeye anajua anapelekwa kwenye tundu la machinjo. Hiyo ni kweli kabisa. Yeye huendea njia iliyowekwa na Mungu.

³⁷ Hivyo ndivyo binadamu anavyopaswa kufanya siku hizi, sio kukusanywa na tundu fulani la kimadhehebu. Bali ni kuingia kwa njia ambayo Mungu alisema uingie, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Kuzaliwa upya, msongamano wa ufufuo. Si kujiunga na kanisa, kutafadhalisha kutoka nyumba moja hadi nyingine, na kusambaza magazeti; bali ni Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili, kujazwa na Roho Mtakatifu, njia ya Mungu, mtu akijiweka huru na ulimwengu. Vema! Kuamini Neno la Mungu! Saa hiyo imewadia. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuamini.

³⁸ Mwanadamu, huwezi kamwe...Sijali ni watu wangapi wangejaribu kwenda kwenye kidimbwi hicho cha bata huko juu na kusema, “Sasa ngojeni kidogo, ninyi mabata wadogo, nina jambo fulani ninalotaka kuwazungumzia. Tuna bata msomi hapa. Ana Ph.D. na LL.D. Kweli ninawaambia, anaweza kuwaongoza.”

³⁹ Hao mabata wanajua vyema zaidi kuliko hivyo. Naam, bwana. Hawajali kuhusu elimu yake iliyo bora zaidi, chochote kile. Wanaweza kutambua mlio fulani anaotoa. Ni silka. Loo, jamani! Kanisa linapaswa kujua kiasi hicho juu ya Neno la Mungu!

⁴⁰ Ni sauti fulani isiyojulikana. Biblia ilisema, Paulo alisema, “Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani anayeweza kujifanya tayari kwa vita?” Hiyo ni kweli, kama kanisa—kama kanisa likitoe sauti isiyojulikana ya “kujiunga.”

⁴¹ Mungu alisema, “Kuzaliwa!” Vile Kuzaliwa kulivyofanya kule, Kuzaliwa kunafanya vivyo hivyo leo, kwa kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Vile alivyokuwa wakati huo, ndivyo alivyo siku hizi. Waliyofanya wakati huo, ndivyo vile vile tunavyofanya leo. Jinsi walivyompata Yeye kule, ndivyo vivyo hivyo wanavyofanya leo. Jambo lile lile walilo nalo siku ya leo, ndilo walilokwa nalo huko nyuma. Kama tu akija, anakuja kwa njia ile ile. Hiyo ndiyo hiyo njia, njia iliyoandaliwa na Mungu. Haibadiliki kamwe.

⁴² Mabata hawabadiliki kamwe. Wanasongamana kabisa, kila mwaka, wanaenda kaskazini, kusini, na upande wowote wanaokwenda. Wanakusanyika kwa wingi kwanza.

⁴³ Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Yeye hilituma Neno Lake kwa majira yake, kwenye majira hayo, ndipo linadhihirishwa. Wala sijali ni vitu vingine vingapi vinavyoendelea; wakati wanapoona Neno la Mungu lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo,

likithibitishwa na kuahidiwa, hakuna kitu kitakachowazuia. “Bikira atachukua mimba.” Na wakati waliposema . . .

44 “Bwana Mungu wetu atawaondokeshea Nabii mithili yangu,” alisema Musa.

45 Na walipomwona Mtu huyu akija na kufanya mambo aliyofanya, walijua ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi. Wakati Filipo alipoona hilo likitendeka, alisema, “Wewe ni Kristo. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Yeye alijua jambo hilo kwa sababu Neno lilikuwa limeahidi hilo, na lilikuwa liko hai katika siku hiyo. Haidhuru ni Mafarisayo wangapi, Masadukayo, waliokuwa wamesimama hapo karibu, Madaktari wa Thiolojia, hilo halikumzuia hata kidogo, kwa maana alikuwa akiitazamia ishara hiyo. Wakati alipoona ikifanywa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya wakati huo. Hiyo ndiyo waliyokuwa wakiitazamia, njia iliyoandaliwa na Mungu. Naam, Bwana.

46 Sasa usingeweza kumpa bata, elimu. Asingeweza kuipata. Asingeitaka. Hao mabata wengine wasingemfuata, haidhuru alisema alikuwa ana digrii ngapi. “Sasa, hebu angalieni hapa, mimi nilisomea kwenye shule ya mabata. Ninajua yote kuhusu jambo hilo. Nimehitimu. Ninajua mambo yote haya.” Haitafaa kitu hata kidogo. Hakuna mmoja wa hao mabata wengine wangemfuata, kama wao ni mabata halisi, amina, kwa sababu wao wanatazamia ishara fulani. Wanapoona ishara hiyo, wanaiamini.

47 Na ikiwa bata ana njia fulani ya kujua jambo hilo, vipi kuhusu Mkristo aliyezaliwa mara ya pili? Tunapaswa kumjua Yesu Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake. Kweli. Mungu anafanya jambo kwa njia iliyoandaliwa na Mungu.

48 Kumbukeni, elimu isingekuwa ndicho chombo cha kuwaongoza kwenda mahali palipoandaliwa na Mungu. Chombo walicho nacho ni silka. Nao, hao mabata, wanajua ya kwamba silka hiyo itawapeleka hadi mahali palipoandaliwa na Mungu.

49 Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu hulipeleka Kanisa mpaka mahali palipoandaliwa na Mungu. Si kujiunga na kanisa, bali ni kujazwa na Uwepo Wake, kuliona Neno Lake likidhihirishwa, likithibitishwa. Hiyo ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya kanisa, daima, kwa ajili ya watu, kuwafikisha mahali ambapo Mungu amewaandalia. Hivyo ndivyo hasa kanisa linavyopaswa kuwa leo. Sasa, tunajua jambo hilo ni kweli.

50 Hakuna njia iliyo bora zaidi kwa ninii . . . Kamwe hawajapata njia iliyo bora zaidi kwa ajili ya mtoto kupata anachotaka kuliko kukililia. Kama ukimpa kengele, na kusema, “Kadogoo, wewe una umri wa siku tatu tu, lakini sasa unapotaka, unapotaka chupa yako, inua kengele hii na kuipiga,” uone kama litafanikiwa. Halifai kitu. Mtoto mchanga hulilia anachotaka. Hiyo ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu. Kadiri

unavyolia kwa sauti kubwa zaidi. . . Usimchape maskini jamaa huyo mdogo, yeye anafuata tu njia iliyoandaliwa na Mungu. Anataka kitu fulani. Hiyo ni kweli. Ndiyo njia pekee anayojua ya kumwita mama yake; kupaza sauti kwa atakacho, kukililia. Hiyo ni kweli.

⁵¹ Mungu hupendekeza jambo hili kwa watoto Wake. Mungu huridhia jambo hili kwa ajili ya watoto Wake wanaoamini. Yeye alifanya jambo hilo. Si hotuba za kielimu, si baadhi ya thiolojia kuu, thiolojia ya kufundisha. Yeye anataka ninyi mlilie haja zenu. Na hilo ni sawa, lilia hilo! Ninyi ni wagumu mno na ni wakavu, kamwe hamtazipata. Kama uko tayari kuvunjika kidogo, na kulia, Mungu atakupa hilo. Yeye anapenda kuwasikia watoto Wake wakilia. Mlilie Mungu haja zako! Mungu anataka jambo hilo. Hiyo ndiyo njia aliyoiweka. Lilia jambo hilo! Hivyo ndivyo mtoto mchanga anavyolia; hivyo ndivyo Yeye anavyokutaka wewe ulie.

“Kulia kwa muda gani?”

⁵² Mtoto hulua kwa muda gani? Mpaka atakaposhiba. Na hivyo ndivyo Mkristo anayeamini anavyopaswa kufanya, mtoto wa Mungu. Kama ukiona ya kwamba Mungu alifanya ahadi, usiikatie tamaa, lia mpaka itakapojibiwa. Lia mpaka utakapoona Mungu anathibitisha Neno Lake. Mungu anapothibitisha Neno Lake, na kuthibitisha ya kwamba liko hapa, basi haikubidi kulia tena; unayo, ondoka uende zako na kumshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Mpaka utakapofanya jambo hilo, paza sauti mpaka utakapolipata. Ninapenda jambo hilo, kung’ang’ania, kushikilia.

⁵³ Si mmea wa haibridi, si ule unaopaswa kudekezwa na kutomaswatomaswa, na kubebwabebwa. Wakristo ni mali ya Mungu iliyo halisi, ya kweli, iliyojaliwa. Wanapigania nafasi yao, na wanapigana mpaka watakapoondokana na dunia hii. Kila hatua wapigayo ni vita.

⁵⁴ Mungu alimwambia Musa amempa ile nchi. Alimwambia Yoshua, “Kila mahali mguu, ama wayo wa mguu wako, utakapokanyaga, hapo nimekupa wewe.” Iliwabidi kupigania kila inchi ya hiyo. Vivyo hivyo nasi tunapigania kila sehemu ya hiyo ardhi. Si kitu cha kudekezwa na kutomaswatomaswa, na mambo kama hayo, na kusema, “Vema, nitakupeleka kule, nione yale unayowazia juu ya jambo hilo. Utoe maoni yako.” Hiyo siyo njia ya kujia.

⁵⁵ Njoo kwa kudhamiria. Njoo kwamba utakaa pale mpaka jambo hilo litakapokwisha. Kaa pale mpaka Mungu atakapojibu na kuthibitisha. Mtu anayemwamini Mungu, anaweza kuona Uwepo wa Mungu, ahisi Uwepo wa Mungu, afahamu uwepo wa Mungu, na ajue Yeye yupo hapa. Yupo hapa kujibu kila kitu alichokifanyia ahadi katika siku hii. Basi, lia mpaka utakapopata jambo hilo! Mshikilie Yeye. Usiondoke, kama

itakubidi kukaa mchana na usiku. Mungu hataki watoto Wake wasikilize hotuba za elimu. Anawataka waililie, mpaka ahadi Hiyo itakapothibitishwa.

⁵⁶ Ibrahimu hapa alikuwa ana haja ya sadaka ya kuteketezwa. Ni kitu gani kilichotukia? Mungu alimpa mwana-kondoo. Hiyo ilikuwa ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu. Yeye alihitaji sadaka ya kuteketezwa, kwa hiyo Mungu akaitoa. Baadaye, alipaita mahali hapo *Yehova-yire*, “Bwana atajitolea sadaka.”

⁵⁷ Sasa, Ayubu, wakati mmoja, yule nabii mzee, Ayubu. Yeye alikuwa ni nabii. Alikuwa ameingia katika shida. Shetani alikuwa ametamani kumjaribu, naye akampiga kwa majipu. Ndipo akawachukua watoto wake, akaichukua mifugo yake, akachukua yote aliyokuwa nayo, kisha akampiga kwa majipu.

⁵⁸ Ndipo wafariji wake wakaja, nao walifanya nini? Hawakutoa kitu chochote ila dharau, wakamtania, wakimwambia, “Ona sasa, umetenda dhambi, kisiri.”

⁵⁹ Naye Ayubu alidumu tu kushikilia. Alipaza sauti. Alikuwa na hakika alikuwa akifuata amri za Mungu. Alikuwa amefanya vile vile hasa Mungu alivyoahidi kufanya. Yale Mungu aliyomwahidi, kwamba angemtetea, chini ya sadaka ya kuteketezwa, naye akakaa pale.

⁶⁰ Kwa hiyo, Mungu alimpa ono. Yeye alikuwa ni nabii. Aliona nini? Aliona Neno, Yesu Kristo. Akasema, “Ninajua Mteteaji wangu yu hai. Na katika siku za mwisho, Yeye atasimama juu ya nchi. Hata mabuu ya ngozi yakiuagamiza mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Unaona, Yeye alimpa ono la ufufuo. Yeye akiwa ni nabii, aliliona Neno. Aliliona Neno na kujua ya kwamba mifupa yake na mwili wake ungefufuka tena katika siku ya mwisho. Aliulizwa kama alijua mahali Mungu alikokuwa, kama angeweza tu kuona.

⁶¹ Akasema, “Ua hufa, hufufuka tena; mti hushuka chini, husimama tena; bali mwanadamu hulala na kutoa roho yake, anaharibika, yuko wapi? Laiti ungalinificha katika kaburi, na kuniweka katika mahali pa siri mpaka ghadhabu Yako itakapopita.”

⁶² Ndipo ngurumo zikaanza kunguruma, umeme ukaanza kumulika, Roho wa Bwana akamjia nabii. Ndipo akasimama, naye akaona kule Kuja kwa Bwana, naye akapaza sauti, “Ninajua Mteteaji wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Mungu alitoa Neno, Yesu Kristo, naye akamwona na akamwita Mteteaji Wake.

⁶³ Israeli walihitaji njia ya kutoka Misri, na Mungu akawapa nabii, nabii aliyethibitisha Neno lililoahidiwa kwa Ibrahimu. Sawa kabisa, njia iliyowekwa na Mungu! Hawakuweza kufunza askari, hawakuweza kufanya *hivi*, hawakuweza

kufanya *vile*. Jambo pekee walilofanya lilikuwa ni kuingojea njia iliyoandaliwa na Mungu. Naye akawaambia, akasema, “Angewatoa watu hao, baada ya miaka mia nne. Watu Wake wangekuwa utumwani, bali Yeye angewatoa kwa mkono wenye nguvu. Angeonyesha ishara Zake na maajabu, na kujipatia utukufu katika taifa hilo.”

64 Huyu hapa mtu huyo akashuka, wakati walipolia na kulia! Na sasa kumbukeni, kulia huko kote kusingewakomboa, mpaka wakati huo ulipotimiza.

65 Mambo haya tunayoona leo, yasingetukia miaka ishirini iliyopita, ama miaka arobaini iliyopita. Leo ndipo yanatukia. Hii ndiyo ile saa! Wakati ndio huu! Sasa wakati huo umetimia. Kwa nini? Mungu aliahidi jambo hilo, nalo liko hapa.

66 Wao walisema, miaka mia moja iliyopita, ya kwamba, “Ubatizo wa Roho Mtakatifu usingewezekana tena.” Walisema, miaka hamsini iliyopita, “Roho Mtakatifu...” Lakini ninyi watu wa Kipentekoste mliwathibitishia, ya kwamba ilikuwa ndiyo saa ya Mungu ya kummwaga Roho Mtakatifu. Haidhuru Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mluteri alivyosema, mlshikilia moja kwa moja Neno la Mungu. Watu hodari walitoka wakaenda huko na kushikilia mpaka ubatizo wa Roho Mtakatifu ukaja, nao wakanena kwa lugha na kumtukuza Mungu. Hakuna mtu anayeweza kuwaambia vinginevyo. Mungu ndiye anayejifasiria; mmelipata. Huenda msiweze kuelezea jambo hilo, bali mnajua mnalo. Ni nani anayeweza kumwelezea Mungu? Hakuna mtu anayeweza.

67 Siwezi kuwaambia jinsi Mungu anavyoweza kuonyesha ono, bali ninajua linatukia. Siwezi kuona jinsi Mungu anavyoweza kufanya mambo haya. Si kazi yangu kuelezea jambo hilo. Yeye ni, anaishi peke yake. Yeye ni Elohimu, Anayejitosheleza. Mimi ni mtumishi Wake tu. Ninajua aliahidi jambo hilo, na ninajua liko hapa. Hilo ni jambo moja ninalojua. Ninajua jambo hilo, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninajua ya kwamba aliahidi jambo hili, na Mungu yupo hapa kuifanya ahadi Yake kuwa ni ya kweli. Naam. Njia iliyoandaliwa na Mungu!

68 Israeli walipewa nabii, aliyethibitisha Neno, nao walitolewa. Nabii huyu, Musa, aliishi kwa miaka kadhaa huko nyikani, miaka arobaini, akishindana na watu hawa, akijaribu kuwaweka mpaka atakapoweza kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Ilifikia mahali, ilibidi mtu huyo kufa; alikuwa na umri wa miaka mia moja na ishirini. Hapakuwapo na mahali pa yeye kufia. Alipokuwa tayari kufa, Mungu akamwandalia Mwamba; Mwamba ule aliokuwa ameupiga huko jangwani, ule Mwamba uliowafuata, waliounywea. Mungu alimpa Mwamba, mahali pa kufia, ambapo Musa angaliweza kufa kifo kizuri.

⁶⁹ Juu ya Mwamba huu, Mungu, jalia nifie kwenye Mwamba uo huo! Hapo ndipo ninapotaka kufia. Mwamba huo ulikuwa ni Kristo Yesu. Naam, bwana.

⁷⁰ Baada ya yeye kufa, juu ya Mwamba huo, alihitaji wabeba jeneza. Mungu alimtumia kundi la Malaika. Kwa nini si kundi la wazee wake? Kwa sababu hakuna mtu angaliweza kumpeleka mahali alikokuwa akienda, ila Malaika. Walimchukua wakampeleka Mbele za Mungu, alihitaji wabeba jeneza na Mungu akamwandalia hilo. Yeye alienda kwa njia iliyoandaliwa na Mungu. Haleluya!

⁷¹ Henoko alikuwa ametembea kwa muda wa miaka mia tano pamoja na Mungu, naye alimpendeza. Alihitaji njia kuu ya kupita kwenda Nyumbani. Mungu aliiandaa.

⁷² Eliya alikuwa amemlaani Yezebeli kuhusu uso wake uliopakwa rangi, na mwenendo wake jinsi alivyowafanya watu wote kufanya. Naye alikuwa amechoka na kudhoofika, na alikuwa karibu yuko tayari kwenda Nyumbani. Alikuwa ni mzee sana hata ilikuwa ni vigumu kwake kwenda kwa miguu kuvuka Yordani; Mungu alimwandalia njia ya kuvuka Yordani. Alitaka kupaa kwenda Mbinguni, afike kwa Mungu; Mungu alishusha gari la moto, na farasi, akamtwaa juu. Njia iliyowekwa na Mungu. Njia iliyowekwa na Mungu. Yeye daima hufanya jambo hilo vivyo hivyo hasa. Sawa. Naam, bwana. Mungu huandaa njia, sikuzote. Naam.

⁷³ Mamajusi, walipokuwa wakija kutoka huko Babeli, walikuwa wakiona njia waliyokuwa wakitaka kupitia, maana walijua Mfalme huyu alikuwa azaliwe. Walihitaji dira; Mungu akawapa Nyota. Waliacha nyuma kila kitu. Hawakuhitaji dira; waliifuata ile Nyota. Ilikuwa ndiyo njia iliyoandaliwa na Mungu. Mungu aliandaa njia, waliifuata hiyo Nyota mpaka wakaiona ile Nuru halisi. Loo!

⁷⁴ Ulimwengu ulihitaji Mwokozi, siku moja. Walikuwa wamepotea; hawakujua jambo hilo. Walifikiri walikuwa wameokoka, bali walihitaji Mwokozi. Mungu aliwaandalia Mwana, kwa ajili ya Mwokozi. Kwa nini? Hakuna mtu mwingine yeyote angaliweza kufanya jambo hilo. Hapakuwa na mtu duniani, hakuna mtu Mbinguni, mahali popote, aliyeweza kufanya jambo hilo. Mungu alimtia uvuli bikira, akachukua mimba na kumzaa Mtoto Mwanamume. Naye huyo Mtoto Mwanamume hakuwa ni Myahudi wala Mmataifa. Yeye alikuwa ni Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, Yeye yule tu ambaye angaliweza kukomboa. Damu Yake hutuokoa sisi. Damu Yake hutuponya. Hiyo Damu ndiyo tunayoweza kutegemea, kwa ahadi yoyote aliyofanya Yeye. Mungu aliahidi kufanya jambo hilo.

⁷⁵ Mungu hukutana tu na mwabuduo kupitia hiyo Damu, na chini ya hiyo Damu. Israeli ilikuwa na mahali pamoja pa

kukutana na Mungu. Si katika ninii...Mungu ana Mahali pamoja, leo, ambapo Yeye—Yeye hukutana na mwabuduo; si kwa Methodist, Baptisti, au Pentekoste. Yeye hukutana nao chini ya Damu. Hapo ndipo mahali pekee palipoandaliwa alipo napo Mungu; si katika madhehebu, si katika shirika fulani. Lakini katika Damu ndipo mahali Yesu Kristo anapokutana na mwabuduo Wake. “Nionapo ile Damu!” Hiyo ndiyo njia iliyowekwa na Mungu.

⁷⁶ Baada ya kanisa kushawishika kabisa, walipomwona Yeye, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi!

⁷⁷ Wakati maskini mwanamke yule pale kisimani, wakati alipohitaji Mwokozi, alihitaji jambo fulani la kuonyesha. Alikuwa amehudhuria kanisani na chochote kile, nao walikuwa wameona kanuni hii ya imani na kanuni ile ya imani, mpaka, akageuka akawa kahaba. Lilimfanya kuingia mtaani. Siku moja, alikuwa akienda kuchota ndoo ya maji, yapata saa tano mchana, na kulikuwako na Mtu ameketi; Myahudi hapa juu, kwenye mandhari ndogo. Na mwanamke huyo akasema. . .

⁷⁸ Wakati alipokwenda kwanza kushusha ndoo yake chini aliyofunga kwenye silingi, apate kuchota maji, alimsikia Mtu mmoja akisema, “Mama, nipe maji ninywe.” Naye akasema. . .

⁷⁹ Aligeuka upesi, na akimwazia kwamba Yeye ni Myahudi wa kawaida tu, kwa kuwa alikuwa ni mwanadamu kadiri inavyohusu habari za mwili. Alikuwa ni Mwanadamu; alikula, alikunywa, alilala, kama sisi nasi tufanyavyo. Alikuwa ni mwanadamu sana hata angeweza kufa, na hata hivyo alikuwa ni Mungu. Ndipo tunaona, ya kwamba wakati. . .

⁸⁰ Kasema “Si kawaida kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria vitu kama hivyo.”

⁸¹ Yeye akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani uliyekuwa ukiongea Naye, ungeniomba Mimi nikupe maji unywe.” Kasema, “Nenda ukamlete mume wako mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

⁸² Akasema, “Umesema kweli. Una watano, na yule unayeishi naye siye wako.” Ni kitu gani kilichotukia? Mungu alikuwa amemwandalia kitu fulani.

⁸³ Akasema, “Bwana, naona ya kwamba Wewe u nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya. Hivyo ndivyo atakavyofanya. Neno linasema hivyo. Tunatarajia jambo hilo. Mimi nimechefukwa na moyo na nimechoshwa na upuuzi huu wote, kanuni zao za imani na kadhalika, Mafarisayo, Masadukayo, na Maherodi, chochote kile. Bali tunajua kuna Masihi mmoja yuaja, wakati Yeye atakapokuja. Unasemaje juu ya jambo hilo?”

⁸⁴ Yeye akasema, “Mimi Ndiye.” Amina! Mungu alikuwa ameweka njia. Akaacha mtungi wa maji, akiwa ni mwanamke

aliyebadilika, kisha akakimbilia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

⁸⁵ Petro, akiisikiliza hadhithi ya Andrea, na alikuwa ameisikiliza mara nyingi, alimsikia Andrea akizungumza habari za Yohana akimtambulisha Masihi, na Mtu mmoja, na mambo haya yote yanayotukia. Yote yalikuwa ni maajabu kwa Petro. Bali siku moja alikuja pamoja na Andrea, kumwona Yesu. Na wakati alipofika Mbele za Yesu, Yesu alimwangalia, na akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Mungu alikuwa amemwandalia Petro njia kuona kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Alikuwa ni huyo Masihi.

⁸⁶ Sasa tunaona, ya kwamba baada ya Yesu kufa, na kupaa Mbinguni, Kanisa lilihitaji Nguvu, kushuhudia. Mungu aliwapa Pentekoste. Aliandaa Pentekoste.

⁸⁷ Miaka elfu mbili imepita, enyi marafiki. Miaka elfu mbili imepita. Katika siku hizi za mwisho, tumekuwa na ninii sana, mwanadamu ameingia katika mfumo wa Ukristo na ameupotosha tena, akauhaibridi kwenye kanuni za imani, makanisa, madhehebu, hotuba za kielimu, mpaka zile Nguvu na jambo halisi la Injili ya Kristo vimepotea kabisa. Na tupo hapa na Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hizi za mwisho, jambo gani litakalotukia, ni nini kitakachotukia; mwanadamu haamini jambo Hilo. Wameliacha. Hebu waulize kama wao ni Wakristo; wanasema, “Mimi ni mfuasi wa *fulani*.” Hilo halimaanishi kitu. Unapaswa kuwa Mkristo kwa kuzaliwa. Sasa tumeweka kitu hicho chote katika Babeli tena, baada ya miaka elfu mbili.

⁸⁸ Kanisa siku hizi linahitaji Nguvu na Kweli, tena. Loo! Mungu alimfufua Mwanawe, kusudi jambo hili lishughulikiwe, kwa kuwa Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Tunaona, katika Waebrania 13:8, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁸⁹ Tunaona, katika Malaki 4, ya kwamba Yeye alituahidi Ujumbe katika siku za mwisho, ambao “ungeirudisha Imani ya watu iwarudie baba zao tena.” Aliahidi jambo hilo, katika siku za mwisho.

⁹⁰ Yeye pia aliahidi, katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Hata nyingi kuliko hizi, ama kuu kuliko hizi, yeye atazifanya, kwa kuwa Mimi ninaenda kwa Baba.”

⁹¹ Alikuwa akizungumza siku moja. Wao wakasema, “Bwana, utuonyeshe sisi ishara.”

⁹² Yeye akasema, “Kizazi dhaifu na cha zinaa kinatafuta ishara.” Hicho ndicho kizazi tunachoishi leo. Yeye alisema, “Nami nitawapa ishara. Kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu usiku na mchana, vivyo

hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi, siku tatu usiku na mchana.”

⁹³ Kizazi kiovu na cha zinaa kingeona ishara ya aina gani? Ishara ya kufufuka. Na hiyo ndiyo tumeahidiwa siku hizi, ishara ya kufufuka ya kwamba Yeye angali yu hai, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁹⁴ Alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu,” kama tulivyolipitia jana usiku. “Siku za Lutu, ni mambo gani yaliyotukia katika siku za Lutu, ndivyo itakavokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Mambo haya tumeahidiwa, maandiko mengi zaidi. Kusudi tusichukue wakati. . . “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena. *Kosmos*, ‘utaratibu, wakati wa kanisa,’ hawataniona tena. Hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ni kitu gani? Ni ishara iliyoandaliwa na Mungu, njia iliyoandaliwa na Mungu.

⁹⁵ Ibrahimu akimngojea yule mwana. Ile ishara ya mwisho aliyoiona kabla ya kuangamizwa kwa Mataifa, ilikuwa ni Mungu akidhihirishwa katika mwili wa binadamu, aliyejua siri za moyo wa Sara wakati alipokuwa ndani ya hema. Yesu alisema, “Hiyo itarudi tena katika kule kuja kwa Mwana wa Adamu.” Ndugu, dada, ninaamini tunaishi katika siku hiyo. Ninaamini ya kwamba hii ndiyo siku hiyo ya ahadi.

⁹⁶ Inakubidi uwe na imani katika yale unayofanya. Endapo huna imani, kama unalichukulia tu kwa kujasiria. . . Neno *kujasiria*, kulingana na webster, maana yake ni, “kudiriki bila mamlaka.” Lakini wakati Neno linapoahidi jambo hilo, Na Mungu anasimama nyuma ya Neno hilo, hujasirii tena. Unafanya vile hasa Mungu alisema ufanye, Naye anawajibika kuunga mkono jambo Hilo.

⁹⁷ Mwa—mwanauamsho mashuhuri, anayejulikana sana, miaka kadhaa iliyopita, nilimwona nilipokuwa mvulana mdogo, alikuwa Paul Rader. Alisimulia hadhithi, siku moja, ambayo daima imenikaa. Alisema, “Siku moja, tulikuwa tukikata miti.” Yeye alikuwa ni mkata miti, huko Oregon, naye akasema bosi alimwambia apande juu ya kilima. Alikuwa anaota. Mahali alipokuwa hasa, wakati huo, alikuwa huko chini visiwani; naye akashikwa na homa, joto kali, naye alikuwa anakufa. Walienda kumtafuta daktari, bali ilikuwa ni umbali wa maili kadha wa kadha, kwa mtumbwi.

⁹⁸ Kabla daktari hajaweza kufika pale, Paulo alianza kudhoofika, akazidi kuwa mgonjwa zaidi. Akamwita mke wake mwaminifu. Akasema, “Mpenzi, chumba kinakuwa na giza, kinazidi kuwa na giza, giza linaingia.” Ndipo akazirai.

⁹⁹ Ndipo alipozirai, alisema aliota ndoto, alipokuwa katika kuzirai huku, ya kwamba bosi wake alimtuma apande

kwenda kukata mti fulani. Aliupata mti huo, akauangusha, akalichomeka shoka lake kwenye mti huo, kisha akanyosha mkono aubebe. Asingeweza kuubeba. Alisema nguvu zake zilimwishia. Asingeweza kabisa kuubeba. Akasema, “Ukubwa wote wa mti huo, hakika ninaweza kuubeba. Hebu nijaribu tena.” Ndipo akainama na akauinua, alisumbuka sana mpaka akachoka kabisa. Akaketi karibu na huo mti, na kusema, “Hata sijui kabisa la kufanya. Bosi anautaka mti huu kule chini kambini, nami nimedhoofu sana siwezi kuushusha huko.”

¹⁰⁰ Kasema alisikia Sauti tamu sana aliyopata kusikia, ilikuwa ni bosi wake aliyenena; bali alisema, alipogeuka kuona bosi wake alikuwa ni nani, alikuwa ni Bwana Yesu. Akasema, “Paulo, unasumbuka sana hivyo kitu gani? Unahangaika sana hivyo kitu gani? Je! unaona yale maji yanayopita pale kasi?” Kasema, “Mbona usilitupe tu gogo hilo mtoni, na kulipanda? Lipande’ mpaka kambini.”

¹⁰¹ Alirukia juu ya hilo gogo na akashuka kwenda juu ya mawimbi, akipiga makelele kwa sauti yake yote. “Ninaliendesha! Ninaliendesha!”

¹⁰² Ndugu, dada, Yesu Kristo aliahidi mambo haya kutukia katika siku za mwisho. Ninaamini ya kwamba tunaishi hapa. Ninaamini ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sijui jinsi jambo hilo lilivyotukia, bali ninaliendesha. Ninaamini ya kwamba ni Kweli, kwa sababu Hiyo ni Injili, njia iliyoandaliwa na Mungu. Ninaamini ni Ujumbe wa wakati huu, saa tunaoishi. Ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Ninasafiri katika Hiyo.

Mbona usirukie juu upande pamoja nami, tunapoinamisha vichwa vyetu?

¹⁰³ Baba wa Mbinguni, tunasafiri kuingia Utukufuni juu ya Neno Lako. Tunaamini ya kwamba Neno Lako ni Kweli. Ee Mungu, jalia kila mwanaume na mwanamke, usiku wa leo, apande aingie kwenye Neno, na akumbuke, wakati wanapoendelea na safari, wanaweza kukiri, “Ninasafiri katika ahadi ya Mungu. Itanipeleka moja kwa moja kuniingiza Utukufuni. Ni njia iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili yangu leo. ‘Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.’”

¹⁰⁴ Ulisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona; kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu.” Ulituahidi, Bwana, tungekuona Wewe.

¹⁰⁵ Wayunani walikuja, wakati mmoja, na kusema, “Mabwana, tungetaka kumwona Yesu.” Nao walipewa majaliwa hayo. Na usiku wa leo, Bwana, tunataka kukuona Wewe, nasi pia. Ni shauku ya mioyo yetu. Hakuna mtu anayeweza kusikia habari Zako, pasipo kutaka kukuona Wewe. Basi kama Wayunani hawa waliruhusiwa kukuona, Nawe ulituandalia njia ya kukuona, Wewe daima unaiandaa njia kwa sababu ni wewe yule jana, leo,

na hata milele. Mtumishi aliwaleta Wayunani hawa Mbele Zako, nao wakakuona. Tupe majaliwa yayo hayo usiku wa leo, Baba. Tujalie, kama watumishi, kulileta kusanyiko hili Mbele Zako. Na jalia tumwone Yesu, usiku wa leo, Ambaye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tujalie, Bwana.

¹⁰⁶ Waokoe waliopotea, Bwana, kama kuna mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana. Tunapolioana taifa letu limechafuka sana kwa wauaji na wakatili, na wachafu, na kuona ufisadi nchini leo! Na kuona ufisadi makanisani, na kuwaona wakielekea kwenye yale machinjo ya ekumeni mwishoni kule, kwa maana hawafuati njia iliyoandaliwa na Mungu! Wanafuata njia ya kanuni fulani ya imani badala ya kufuata Neno.

¹⁰⁷ Mungu, tunaomba ya kwamba Wakristo halisi, wa kweli, waliozaliwa mara ya pili, kama nilivyolionyesha, kwa wao kuwa mabata halisi, wao. . . “Kondoo Wangu wanaisikia Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata.” Bwana, Sauti Yako ni Neno. Hiyo daima imekuwa ndiyo njia uliyoandaa kwa ajili ya Kanisa na kwa ajili ya watu, ni Neno Lako. “Neno Lako ni Kweli.” Nawe ni Neno. Na Biblia inatwambia, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.”

¹⁰⁸ Kwa nini Israeli hawakuweza kumwona Masihi wao, wakati walipoota ya kwamba Yeye alikuwa ndiye hilo Neno, wakati Yeye aliweza kuyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao? Kwa nini hawakumtambua? Walifahamu jambo hilo kupitia kwa manabii, ya kwamba manabii waliweza kutambua mawazo; bali wakati utimilifu wa Mungu ulipofanyika Mwanawe, Naye akaishi miongoni mwetu, ndipo walishindwa kuona hilo kwa kuwa walikuwa wamepofushwa.

¹⁰⁹ Bwana, wale walioyafungua macho yao, usiku wa leo, jalia tumwone Yesu miongoni mwetu. Jalia kila mgonjwa aponywe. Jalia hili litatue jambo hili, Bwana, ya kwamba wao kamwe hawataweza, tena, tangu saa hii na kuendelea. . . ila wale watakaomini ya kwamba Wewe ni Masihi. Wanakuja kwa njia ya Mungu. Wengi wao wako hapa, usiku wa leo, wakifa. Wapo wengi hapa, usiku wa leo, ambao labda hawatakuwa hapa juma moja tangu sasa, kama Wewe, msaada Wako hautakuja.

¹¹⁰ Sasa, Baba, Wewe unawajibika tu kwa yale uliyoahidi. Bali uliahidi ya kwamba sisi tungekuona. Uliahidi ya kwamba yale uliyofanya sisi nasi tungeyafanya pia. Hii ndiyo hiyo saa. Nimekiri jambo hilo; ninaliamini. Nilikusikia ukisema hivyo; Neno Lako linasema hivyo. Unalithibitisha. Ninajua ni kweli. Sasa hebu na ijulikane, Bwana. Limeandikwa, sasa hebu na lifanyike, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Amina.

¹¹¹ Sidhani tutafanya mstari wa maombi. Ninaamini nitaufanya tu toka papa hapa.

¹¹² Ni wangapi wenu ambao ni wagonjwa? Sasa hivi mtaninii. . . Unainua mkono wako, ukishuhudia wewe ni mgonjwa.

¹¹³ Ni wangapi wenu watashuhudia jambo lile lile, “Ndugu Branham, kwa kweli mimi sijaokoka”? Waweza kuinua mkono wako, “Niombee”? Mungu akubariki wewe, wewe. Hilo ni zuri. Hilo ni . . . Mungu akubariki. “Mimi sijaokoka.”

¹¹⁴ Sasa, ninyi mlioinua mikono yenu, na ninyi ambao hamkuinua, “Lakini, Ndugu Branham hakika ninataka kuokoka. Liko moyoni mwangu. Ninaamini ya kwamba hakuna kilichosalia kwa yeyote yule ulimwenguni.” Ni nini zaidi, ungeweza kupata nini, ambacho kingekuwa ni kikuu zaidi ya wokovu wako? “Niombee. Ninataka kuokolewa.” Je! waweza kuinua mkono wako, Kote jengoni, popote, “Ninataka. . . .”?

¹¹⁵ Ni wangapi wenu hawajampokea Roho Mtakatifu, waseme, “Ninajua sina budi kumpokea”? Inueni mikono yenu. “Sijampokea; ninataka kumpokea.” Vema, sio wengi ambao hawajampokea.

¹¹⁶ Sasa, Kristo hutimiza Neno Lake, Nawe huna budi kudumisha imani Yako katika Yeye. Yeye ndiye Neno. Sasa, Waebrania mlango wa 4, ilisema kwamba, “Neno la Mungu,” ambalo ni Kristo. Kristo ni Neno. Nyote mnajua jambo hilo? Semeni “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye ni Neno, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Kile alichokuwa katika Musa, alikuwa pia katika Eliya; kile alichokuwa katika Eliya, alikuwa katika Yohana; alichokuwa katika Yohana, alijikamilisha Mwenyewe katika—katika Yesu. Na leo hii ni yeye yule kama alivyokuwa zamani hizo, na lingali ni Neno la Mungu lililotabiriwa kwa ajili ya siku hii, jambo ambalo linamfanya Yeye kuwa Nuru inayomulika na kuthibitisha Neno lililoahidiwa.

¹¹⁷ Tuko katika wakati wa mwisho, wapendwa. Yesu yupo. Ninajua mmesikia jambo hilo.

¹¹⁸ Vipi kama hujapata kuona, maishani mwako, wala kamwe hujawahi kuwa na hisi ya kuona, hakuna mwanadamu aliyepata kuwa nayo, lakini mara mojamoja ulihisi hisi halisi yenye joto? Nami nilikuwa na macho, ningeweza kuona, nami ningekwambia ilikuwa ni jua. Ungesema, “Sijui jinsi jambo hilo linavyotukia, bali ninahisi, kama joto, unaweza kuhisi.”

Niseme, “Hilo ni jua.”

“Jua ni kitu gani?”

“Ni nuru.”

“Nuru ni nini?” Ungekuwa ni ulimwengu mpya kabisa kwako.

¹¹⁹ Lakini vipi kama ningalikwambia Yesu Kristo alikuwa amesimama hapa sasa? Vipi kama ningalikwambia Yeye yuko miongoni mwetu? Aliahidi jambo hilo. “Walipo wawili ama watatu wamekusanyika katika Jina Langu, Mimi huyo hapo miongoni mwao. Nipo hapo!” Sasa hilo ama ni Kweli, kwangu

mimi, *Hili* lote ni Kweli, ama si Kweli kamwe. *Hili* aidha ni Kweli, ama si kweli.

¹²⁰ Sasa, kuhusu kukuokoa, Yeye alifanya jambo hilo wakati alipokufa hapo Kalvari. Kukuponya, Yeye alifanya hivyo hapo alipokufa pale Kalvari. Amini jambo hilo. Neno lilisema alikuponya.

¹²¹ Sasa jambo pekee ambalo angeweza kufanya, kama angekuwa amesimama hapa akiwa—akiwa amevaa suti hii, ambayo alinipa, ingekuwa tu ni kukuthibitishia Yeye ni Masihi.

¹²² Si kwa makovu ya misumari mkononi Mwake. Mnafiki yeyote anaweza kufanya jambo hilo, kuweka makovu ya misumari, na damu juu ya uso wake, na alama na kadhalika. Hilo linaweza kufanyika. Hilo lilikwishafanywa. Watu wengi hata walipata kusulibishwa kama alivyosulubishwa Yeye. Hilo silo.

¹²³ Bali Uzima Wake, kile kilichokuwa ndani Yake! “Mwana hawezi kufanya neno, Yeye Mwenyewe, ila lile analoona Baba akifanya.” Ni huo Uzima ulio ndani Yake, ambao umelithibitisha. Si kwa sababu eti alikuwa ni Myahudi kwamba maskini yule mwanamke kisimani akamwamini kwamba ni Masihi; ni kwa sababu angeweza kuyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwake, hilo ndilo lililomfanya Yeye kuwa Masihi. Kama hivyo ndivyo Masihi alivyojitambulisha Mwenyewe katika siku zilizopita, hiyo ilikuwa ndiyo njia Yake iliyoandaliwa ya kujitambulisha. Hiyo ndiyo njia Yake iliyoandaliwa, kulingana na Maandiko, kwa ajili ya wakati huu. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹²⁴ Sasa, kila mmoja wenu hapa, mimi ni mgeni. Nimeangalia pande zote, sioni mtu ninayemjua. Kila mtu ndani hapa, ambaye hanijui, na anajua mimi sijui lolote kukuhusu wewe, inueni mikono yenu. Wengi mno, kila mahali. Mtu huyu anayelala hapa kwenye machela, aliinua mkono wake. Hakunijua mimi. Hakuna mtu anayenijua mimi.

¹²⁵ Lakini kumbukeni, Mungu anawajua. Mungu anawajua. Sasa, kama Yeye akithibitisha ya kwamba yuko hapa.

“Ni kitu gani, Ndugu Branham?” Ni karama.

¹²⁶ Karama ni nini? Karama ni kitu gani, hata hivyo? Si kuchukua kitu na kutumia kitu, useme, “Nina karama ya uponyaji! Ninatoka kwenda na kumponya *huyu*, ninamponya *yule*.” Kama ningaliweza, hakika nigalifanya jambo hilo. Sasa, lakini, karama, na ninyi mna—mnaninii. . . Mnafasiri karama vibaya. Karama ni “kujiondoa tu njiani na kumruhusu Roho Mtakatifu akutumie.” Unaona? Hiy ndiyo karama.

¹²⁷ Hivyo ndivyo mhudumu alivyo. Yeye hahubiri kile anachotaka kuhubiri. Yeye anajiondoa njiani tu, ni karama, ndipo uvuvio huja, naye—naye anazungumza kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Karama nyingine yoyote ni vile vile. Sasa,

karama za kuhudumu, na kadhalika, zimekwisha kuwapo. Kuna, kwanza, karama zilizotolewa na Mungu, ni, “kwanza mitume, manabii, waalimu, wachungaji, na wainjilisti.” Hizo ndizo afisi. Hizo ndizo karama zetu.

¹²⁸ Sasa, Yesu Kristo aliahidi ya kwamba angefanya jambo hili katika siku za mwisho. Kama akifanya hilo, kama akiahidi jambo hilo na atalitekeleza, ni wangapi watakaoamini na kumkubali Yeye, usiku wa leo? Inua mkono wako, useme, “Nitamkubali.” Ni wangapi waliopo hapa ndani basi... Asanteni. Ni wangapi waliopo hapa ndani ambao hawajapata kuhudhuria katika mmoja wa mikutano hii hapo kabla, inua mkono wako. Jamani, karibu nusu ya umati huu. Ni wangapi wanaoamni, kabla Yeye hajafanya jambo hilo, mnaamini hata hivyo? Mungu awabariki.

¹²⁹ Sasa angalia. Kama nimewaambia Kweli, Mungu anawajibika kunijibu mimi. Atanijibu. Anaweka Maneno Yake kinywani mwako Nayo yanaumba kitu. Hiyo ni kweli, ni Maneno Yake. Halina budi kutenda hivyo. “Nimelituma Neno Langu, halitarudi bure.”

¹³⁰ Sasa, kama ningaliweza kuponya, ningefanya hivyo. Ni kama tu yule mheshimiwa, hayati, Ndugu Upshaw ambaye tulikuwa tukinena habari zake. Maskini mzee huyo akiketi kule nyuma kwenye kiti hicho cha magurudumu, mzee shujaa, ningalimponya kama ningaliweza. Nilianza kuondoka jukwaani, kusema kweli, ndipo nikageuka na kumwona katika ono, akienda, akitembea. Nikamwita, nikamwambia kwamba ilikuwa ni kitu gani, na hayo yalikuwa ni kweli tupu. Aliamka na akatembea, akaja jukwaani, akagusa vidole vyake vya miguu, baada ya kuwa kilema kwa muda wa miaka sitini na sita. Unaona?

¹³¹ Usiku huo huo, bibi mweusi, akiwa na mtoto wake mchanga, wakiwa huko chini pembeni. Nikasema, “Ninamwona da—daktari amevaa miwani na—na amemfanyia upasuaji maskini msichana huyo mweusi, na huo umempoozesha kuanzia kooni mwake.”

¹³² Maskini mwanamke mweusi mzee, ilikuwa ni vigumu kumwondoa jukwaani. Yeye alisema, “Bwana, rehema, huyo ni mtoto wangu mchanga!” Naye huyu hapa anakuja, kundi la mabawabu hawakuweza hata kumshika.

¹³³ Nikasema, “Shangazi, haitakusaidia chochote kuja huku juu. Hiyo siyo... Huyo ni Mungu.” Nikasema, “Haitafaa kitu kuja hapa. Amini tu.” Naye akapiga magoti na kuanza kuomba. Nikaangalia kwa wasikilizaji nami nikaona kichochoro, kitu kama hicho, kikiendelea. Nikaona maskini msichana mdogo mweusi akiwa na mwanasesere mikononi mwake, akitembea kwenye kile kichochoro. Nami nikamwangalia maskini msichana huyo mdogo, mweusi, nikaangalia nyuma,

na alikuwa ndiye mwenyewe. Nikasema, “Imejibiwa.” Huyoo akaruka, na akatoka kwenye machela. Unaona?

¹³⁴ Ni Mungu. Unaona? Ni Mungu. Unaona? Yeye hawezi... Hakuna mtu anayeweza kuponya. Ni imani yako katika Mungu.

¹³⁵ Sasa, Biblia ilisema, ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuchukuana nasi katika hali ya udhaifu wetu.” Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kuhani Mkuu! Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu, yeye angefanyaje? Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angetenda vile vile jana, leo, na hata milele.

¹³⁶ Sasa ninyi ombeni, na hebu Roho Mtakatifu basi... Mwambie Mungu, “Mungu, mtu huyu anayesimama pale hanijui mimi, bali anayosema yanaleta maana. Ni wewe yeye yule. Wewe ni Kristo. Mimi ni mgonjwa. Nina haja. Na kama wewe ukindiruhusu aidha... Kama sina imani ya kutimiza jambo hilo, jalia mtu ninayemjua ana imani, na hebu ininii... Wewe ita na jalia—jalia—nijalie mimi ama mtu huyo aguse upindo wa Nguo Yako huko Utukufuni. Basi kama mtu huyo amejiondoa njiani, basi Wewe tumia kinywa chake kuninenea, na lifanye tu namna ile ile ulivyofanya wakati ulipokuwa hapa duniani. Nitajua ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

¹³⁷ Bwana Yesu, nikigeuka kutoka kwenye uinjilisti kuingia katika unabii, bali hata hivyo ninakuamini, Bwana, Wewe uliahidi jambo hilo. Nami ninaomba ya kwamba utatujalia jambo hilo, usiku wa leo. Tujalie. Nisikie. Wakati wasikilizaji hawa watakapoondoka hapa, usiku wa leo, na twende nyumbani, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, “Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Yesu alifufuka kutoka kwa wafu; hawakujua jambo hilo. Walikuwa wakizungumza Naye; hawakujua jambo hilo. Lakini wakati alipokuwa nao ndani ya nyumba ile, na wakafunga mlango, ndipo akafanya jambo fulani jinsi alivyolifanya kabla ya kusulibiwa Kwake. Hilo liliyafungua macho yao. Waliona ilikuwa ni Yeye. Tena, Bwana, jalia mioyo yetu iwakewake tunapokwenda nyumbani usiku wa leo, kama yao ilivyofanya. Kwa kuwa tunajua ya kwamba umesema na sisi njiani. Fanya mambo hayo, usiku wa leo, ambayo ulifanya wakati ulipokuwa duniani, kwa kuwa ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

¹³⁸ Sasa iweni katika maombi na aminini tu. Hebu na tuweke wakfu upande *huu*, kwanza. Haidhuru wewe uko wapi, humu jengoni, mwamini Mungu. Laiti kila mtu angalikuwa na kicho kwelikweli na aketi kimya, aombe.

¹³⁹ Hili haliwezekani kabisa. Nilikuwa nikizungumza asubuhi ya leo, kwenye kiamshakinywa cha wahudumu, “kitendawili.” *Kitendawili* ni kitu kisichoaminika, “kitu kisichoaminika, bali

hata hivyo ni kweli.” Mnajua ya kwamba Roho Mtakatifu angesimama hapa na kusema kitu fulani katika kusanyiko hilo, kwa watu ambao siwajui, itabidi iwe ni kitendawili. Ni kitu kisichoweza kuelezeka. Sijui kwamba atafanya jambo hilo. Ninatumaini tu kwamba atafanya, nikitumaini ya kwamba atafanya.

¹⁴⁰ Sasa hebu tu ombeni tu, na msema, “Bwana Yesu, ninataka kugusa vazi Lako, nami ni—nina haja. Ninakuahidi, Bwana, nita—nitakutumikia maishani mwangu mwote.” Mungu anakutaka wewe utubu. Kama hujatubu; tubu, useme, “Ninataka kutubu, Bwana. Ninakutaka Wewe uniponye. Ninataka Wewe unibariki. Niponye sasa Bwana. Mimi ni mtumishi Wako.”

¹⁴¹ Nilikuwa nikienda... Je! ulisambaza kadi za maombi leo? Nilikuwa tu nikitaka kumwuliza Billy kama... Kama asipofanya hivyo, ningeita mstari wa maombi. Lakini wao hawakusambaza kadi za maombi leo. Ketini tu mkiwa na kicho, mwamini.

¹⁴² Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho hapa chini ya mamlaka yangu, kwa utukufu wa Mungu, kusudi Neno Lake lipate kujulikana, kusudi katika Siku ile ya Hukumu hatutakuwa na udhuru.

¹⁴³ Sasa angalieni huku, na mwamini sasa. Omba kwa moyo wako wote, na uombe tu, na kwa unyenyekevu. Usilipige vita. Wewe tulia tu, na kusema, “Bwana, Wewe ulifanya ahadi hiyo. Ninakuamini.” Hivyo ndivyo inavyonibidi kufanya.

¹⁴⁴ Ninajua hakuna haja ya mimi kuwauliza. Ni wangapi waliowahi kuona ile Nuru? Hebu tuone. Mmeiona picha Yake. Hebu na tuone mikono yenu, waliopata kuona picha Yake. Hivi hamwioni pale kabisa? Unaona, iko katika kiwango kingine. Iko moja kwa moja juu ya mama yule.

¹⁴⁵ Anaugua miguu yake na mgongo. Yeye... Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, dada? Je! uligusa nini? Hunijui, bali uligusa kitu Fulani. Kama Bwana Yesu ataniambia kwamba wewe ni nani, je! hilo litakufanya uamini vizuri zaidi? Wewe ni Bibi Phillips. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Vema. Je! mimi sikufahamu wewe kabisa? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Sijapata kumwona maishani mwangu. Je! aligusa kitu gani? Nenda ukazungumze na mwanamke huyo, baadaye. Maumivu yote yamekwisha sasa. Uko mzima. Unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima.

¹⁴⁶ Huyu hapa bibi mmoja, moja kwa moja nyuma yake hapa. Anaugua ugonjwa wa neva. Ee Mungu, kama haninii... Jina lake ni Bibi Star. Amini, Yesu Kristo atakufanya mzima. Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako. Kama mimi ni mgeni kwako, tikisa mikono yako. Ugonjwa wako wa neva umekwisha. Yesu Kristo anakuponya.

147 Je! Yeye aliahidi nini? Aliliahidi. Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

148 Yupo mama mmoja papo hapo nyuma yake, ameketi pale. Yeye anaomba. Ana wasiwasi, ana matatizo chungu mbovu. Anataka kuacha kuvuta sigara. Jina Lake ni Bi. Bordon. Simama, Bi. Bordon. Sigara zako zimekwisha. Yesu Kristo anakuponya. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu.

149 Je! unaamini? Sasa mnajua siwezi kufanya jambo hilo. Huyo ni Yesu Kristo. Ni kitu gani? "Neno ni jepesi, lina nguvu zaidi, kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Ni Neno, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hivi huwezi kuamini jambo hilo?

150 Hapa, hapa ameketi mtu hukuu, ana ngiri, ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Simjui mtu huyu. Sijapata kumwona. Lakini yeye ni mhudumu. Kasisi, Bw. Kinsey. Hiyo ni kweli. Je! unaamini, bwana? Simama kwa miguu yako na upokee uponyaji wako. Yesu Kristo anakuponya.

151 Licha ya hayo, je! utanipa kibali, kwa kuwa wewe ni mhudumu? Weka mikono yako juu ya mke wako, ana ugonjwa wa figo, pamoja na ini, na uzito uliozidi, pamoja na matatizo mbalimbali. Weka mikono yako juu yake. Utamwacha, kama ukiamini.

152 Aisee, yupo mtu anayeketi papo hapo nyuma yako, ana kivuli cha mauti. Ana kansa. Mtu huyo anaumwa uvimbe, kansa, wasiwasi. Jina lake ni Bw. Young. Amini sasa. Yesu Kristo anakuponya. Je! unaamini hayo? Unakubali hayo? Vema, bwana.

153 Huyu hapa mtu amelala, amelala hapa katika machela hii. Bwana, mimi sikujui. Kama ningaliweza kukuponya, ningefanya hivyo. Wewe hunijui mimi. Umekuja umbali huu wote. Umejithahidi kuja hapa. Huwezi kuficha shida zako; bali siwezi kukuponya. Umekuja hapa pamoja na mke wako. Ndiye yule pale ameketi pale amevaa hilo koti lenye rangi ya tunda la pichi. Hiyo ni kweli. Vyema. Mwanamume huyo amefunikwa na kivuli cha mauti; hawezi kuishi ila kwa muda kidogo sasa. Ana kansa.

154 Unaumwa, pia, dada. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia ugonjwa wako? Ni ugonjwa wako wa mgongo. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, simama. Vema, pokea uponyaji wako. Amini jambo hilo. Weka mkono wako juu ya mume wako.

155 Je! uniamini mimi kuwa nabii Wake, bwana? Kama ukikaa pale, hakika utakufa. Huwezi kuishi. Hivyo tu. Madaktari wamekukatia tamaa. Kansa imekutafuna kabisa. Nimeona magonjwa hatari zaidi kuliko yako yakiponywa. Siwezi kukuponya. Bali kama tu utakubali na kuamini! Unaamini? Ndiyo nafasi yako ya pekee. Nyakati zako za mwisho zinapita. Unaamini? Endapo unaamini, simama utoke kwenye machela

hiyo. Simama utoke hapo, katika Jina la Yesu Kristo! Simama kwa miguu yako na uponywe, na utoke hapa, ukimtukuza Mungu. Mtu fulani na ampe mkono pale, amsaidie. Huyo hapo, amesimama.

¹⁵⁶ Ni wangapi hapa ndani wanaamini? [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.] Inueni mikono yenu. Simama kwa miguu yako. Ninyi wengine mnaotaka kuponywa, simameni, katika Jina la Yesu Kristo. Inueni mikono yenu, msifuni Mungu. Mpeni sifa na utukufu. Sasa mshukuruni Bwana kwa uponyaji wenu, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele!

¹⁵⁷ Ndugu, madaktari wameshindwa. Hii ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Iaminini!

¹⁵⁸ Ni wangapi wanaotaka kuikubali njia iliyoandaliwa na Mungu? Inueni mikono yenu na mumpe Mungu sifa, kila mmoja wenu, na mwamini ya kwamba mmeponywa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.



NJIA ILIYOWEKWA NA MUNGU KWA AJILI YA SIKU HII SWA64-0206E

(God's Provided Way For This Day)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 6 Februari, 1964, katika Uwanja wa Maonyesho wa Wilaya ya Kern, huko Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org